

# HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Jiji)

Simu Mkurugenzi : 255(28) 2501375  
Ofisi zote : 255 (28) 40334  
Fax : 255 (28) 2500785  
E-mail. [cd@mwanzacc.go.tz](mailto:cd@mwanzacc.go.tz)  
[info@mwanzacc.go.tz](mailto:info@mwanzacc.go.tz)



S. L.P. 1333  
**MWANZA.**  
**TANZANIA**

Kumb Na. E.30/1/Vol. IX/ 23

3 Novemba, 2017

## **TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA MSIMAMIZI MSAIDIZI NA. 2 WA KITUO**

1. Msimamizi wa Uchaguzi wa Jimbo la **Nyamagana** anatangaza nafasi za kazi ya **MSIMAMIZI MSAIDIZI NA. 2 WA KITUO CHA KUPIGIA KURA** ambaye atakuwa na jukumu la kusimamia shughuli za uchaguzi na kuhakikisha utulivu na usalama katika kituo cha kupigia kura kwenye Uchaguzi wa Marudio Kata ya Mhandu kujaza nafasi Wazi ya Diwani utakaofanyika **tarehe 26 Novemba, 2017**.

Aidha, majukumu mengine ya Msimamizi Msaidizi Na. 2 wa Kituo ni:-

- Kuhakikisha kuwa anawaelekeza Wapiga Kura kutumbukiza kura zao katika Sanduku husika,
- Kuhakikisha kuwa Wapiga Kura waliokwisha piga kura zao wanapakwa wino usiofutika katika kidole kidogo cha mwisho,
- Atawajibika kwa Msimamizi wa Kituo cha Kupigia Kura.

## **2. SIFA ZA MSIMAMIZI MSAIDIZI NA. 2 WA KITUO CHA KUPIGIA KURA**

- Awe raia wa Tanzania,
- *Ikiwezekana* awe mkazi wa Kata ya MHANDU ambayo atafanya kazi ya kusimamia Upigaji Kura na Kuhesabu Kura,
- Asiwe Kiongozi au Shabiki wa Chama cha Siasa,
- Awe *Mwadilifu, Mvumilivu, Mpole, Mtiifu, Msikivu* anayeweza *kufanya kazi kwa kujituma*,
- Awe na elimu ya Kidato cha nne au zaidi na anayeweza kusoma na kuandika vizuri. Pia anayeweza *kuyaelewa Maelekezo ya Wasimamizi wa Vituo vya Kupigia Kura*,
- Awe na uwezo wa kuelewa vizuri Maelekezo ya Tume

yanayohusu Orodha ya Wapiga kura,

### **3. UTARATIBU WA KUOMBA NAFASI YA KAZI**

Mwombaji anapaswa kuomba nafasi husika akitoa taarifa kamili zinazo mhusu kulingana na sifa zilizotajwa na pia akitaja; kazi yake anayofanya hivi sasa, namba yake ya simu, Jimbo, na Kata anayokaa.

Aidha, Mwombaji ambatanishe picha moja ya rangi yenyeye ukubwa wa pasi ya Kusafiria (passport size), vyeti na kitambulisho chochote alichonacho.

Waombaji walioajiriwa wapitishie maombi yao kwa Waajiri wao.

Maombi yote yatumwe kwa:-

**Msimamizi wa Uchaguzi,  
Jimbo la Nyamagana,  
S.L.P. 1333  
MWANZA**

Maombi ya nafasi ya kazi Msimamizi Msaidizi Na. 2 wa Kituo cha Kupigia Kura yanaweza kuwasilishwa moja kwa moja katika Ofisi ya Msimamizi wa Uchaguzi, Halmashauri ya Jiji la Mwanza.

### **4. MUDA WA MWISHO WA KUWASILISHA MAOMBI (DEADLINE)**

Muda wa mwisho wa kuwasilisha Maombi ya nafasi ya kazi ni tarehe 11/11/2017 saa 9:30 Alasiri.

*KIOMONI KIBURWA KIBAMBA  
MSIMAMIZI WA UCHAGUZI  
JIMBO LA NYAMAGANA*